| | |
|---|---|
| **Jina la Mradi:** | Mradi wa Misitu ya Jamii – MJUMITA (Lindi) |
| **Eneo Ulipo Mradi:** | Wilaya ya Lindi Vijijini na Manispaa ya Lindi, Mkoa wa Lindi, Tanzania |
| **Mmiliki wa Mradi:** | Wamiliki ni wengi (Halmashauri za Vijiji) Wakiwakilishwa na MJUMITA |
| **Mhusika:** | Rahima Njaidi, Mkurugenzi Mtendaji, MJUMITA |
| **Barua-pepe na Simu:** | rnjaidi@gmail.com +255 22 2669007 |
| **Mkaguzi:** | SCS Global Services |
| **Mhusi wa Ukaguzi:** | Francis Eaton, Mratibu, Greenhouse Gas Verification, Natural Resources Division, SCS Global Services |
| **Barua-pepe na Simu:** | FEaton@scsglobalservices.com +1 510 452 8027 |
| **Muda wa Kuanza kwa Mradi:** | Tarehe ya 1 Aprili, 2010 |
| **Muda wa Kupunguza Hewa Ukaa:** | Miaka 30, Tarehe ya 21 Aprili 2012 - Aprili 20' 2042 |
| **Muda wa Mradi:** | Tarehe ya 1 Aprili 2010 na utaendelea hadi Aprili 20 2042 |
| **Uthibitishaji Uliokamilika kwa Kutumia Viwango vya CCB Toleo la 3** | |
| **Historia ya Kuthibitishwa na CCB:** | Uthibitishaji wa Kwanza |
| **Tarehe ya Kukamilika kwa Andiko hili la Mradi:** | Tarehe 18 Aprili 2014 |
| **Utaratibu wa Uhakiki Unaotegemewa:** | Uhakiki wa awali utafanyika pamoja na uthibitishaji wa awali. Uhakiki wa baadaye utafanyika kwa mujibu wa VCS kwa kila kipindi cha miaka 1 – 2. |

**Muhtasari wa manufaa ya tabianchi, jamii na bionuwai yaliyopatikana wakati wa utekelezaji mradi na yaliyoelezwa kwenye taarifa hii ya utekelezaji wa mradi.**

**Manufaa ya tabianchi**
Tani za hewa ukaa 40,178 ziliweza kupatikana kama matokeo ya utekelezaji wa mradi.

**Kiwango cha Dhahabu 1 Faida za Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi:** Uwezo wa jamii kuhimili mabadiliko ya tabianchi uliimarishwa kwa kuanzisha mbinu za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na upatikanaji wa huduma za kuweka na kukopa.

**Manufaa ya jamii**
***Usimamizi wa misitu ya jamii***
Jumla ya hekta 33,726 za misitu ya pwani na misitu ya matajiwazi imetengwa kama misitu ya hifadhi katika vijiji 10 vya mradi. Kamati za maliasili za vijiji zipo katika vijiji 10 ambapo idadi ya wanawake ni ni asilimia 25 % - 55 % ya wajumbe wa kamati.Ufyekaji wa misitu umepungua kuanzia asilimia -1.91 % to -1.58 % katika eneo la mradi (0.92% katika misitu ya hifadhi ya vijiji). Sheria ndogo za vijiji zinatoa mwongozo wa haki za kupata mazao ya misitu kwa wakazi 13,741 wanaoishi katika eneo la mradi.

***Kuimarisha utawala bora na umiliki wa ardhi***
Mafunzo kuhusu utawala bora, dhima na majukumu ya jamii yalitolewa katika vijiji kumi. Kutokana na mafunzo hayo, mikutano ya halmashauri za vijiji na mikutano mikuu ya vijiji inafanyika mara nyingi zaidi. Vijiji vyote kumi sasa vina mipango ya matumizi bora ya ardhi, na migogoro mingi ya mipaka imeshashasuluhishwa.

***Kuimarika kwa ulinzi wa misitu yenye thamani kubwa ya uhifadhi ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji na udongo***
Vyanzo vingi vya maji vimejuishwa katika misitu ya hifadhi ya vijiji, na sheria ndogo za matumizi bora ya ardhi zilizopitishwa hivi karibuni zinalenga kulinda vyanzo vya maji na mito dhidi ya uharibifu. Maeneo mengi yenye miteremko mikali imejumuishwa kwenye misitu ya hifadhi ya vijiji ili kulinda kutokana na ufyekaji wa misitu na hatari ya mmomonyoko wa udongo. Mbinu za usimamizi wa udogo zinafundishwa kama sehemu ya kilimo hifadhi katika vijiji nane.

***Kuimarika kwa hali ya maisha***
Kipato cha mtu mmoja mmoja kiliongezeka kwa kupokea TZS 199,598,000 wakati wa malipo ya majaribio ya MKUHUMI. Haya yalilipwa kwa wanaume 1836 wanawake 2685 na wataoto na wategemezi 5224 katika vijiji nane.
Wakulima wanawake 154 na wanaume 123 wamefundishwa mbinu za kilimo hifadhi ambapo wanawake 6 na wanaume 12 walipewa mafunzo ya ziada kama Maafisa Ugani wa Jamii. Pia wanawake 71 na wanaume 199 wamefundishwa mbinu za ufugaji wa nyuki na wanajamii 264 wamejiunga katika vikundi vya kuweka na kukopa vinavyoendeshwa wanajamii waliofundishwa 30.

***Kuimarika kwa huduma za jamii na miundombinu***
Miradi ya maendeleo ya jamii iliyochaguliwa na wananchi iligharamiwa kwa kutumia fedha za malipo ya majaribio ya MKUHUMI ikijumuisha ujenzi wa madarasa 3 ya shule, zahanati 3 na mtandao mmoja wa maji. Vijiji vyote kumi sasa vina majengo ya ofisi za vijiji. Majengo mengine mawili ya vijiji yalijengwa kwa vijiji vilivyo karibu na eneo la mradi.

**GL2.Manufaa ya pekee ya Jamii:** Faida za jamii zipo katikati ya lengo kuu la mradi. Usanifu wa mradi umekuwa ukiongozwa na wanajamii na ndio wasimamizi wa kisheria wa eneo la mradi. Tangu mradi ulipoanzishwa, mradi ulilenga kuonyesha mbinu rahisi zinazozingatia kuondoa umaskini katika mradi wa MKUHUMI.

**Manufaa ya Bionuwai**
Komba wafupi wa aina ya Rondo galago walinukuliwa tena kutoka katika eneo la mradi; kama kulivyokuwa na aina tatu za mimea iliyo karibu kutoweka na aina nne ya mimea iliyohatarini na hekta 33,726 za misitu iliyo katika tishio kwenye ukanda wa Misitu ya Afrika ya Mashariki inalindwa vizuri kupitia dhana ya usimamizi wa misitu ya jamii.

**GL 3: Manufaa ya pekee ya bionuwai:** Eneo la mradi linajumuisha idadi kubwa ya nyani walio katika hatari ya kutoweka, komba aina ya Rondo galago pamoja na aina tatu ya mimea iliyohatarini kutokweka na aina nne mimea iliyo katika hatari. Kwa kuhifadhi makazi ya aina hii ya viumbe katika eneo la mradi kunalenga kuzuia kupungua kwa viumbe hivi katika eneo hili.

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

## MKUHUMI Unaotekelezwa na Jamii katika Misitu ya Pwani Tanzania

# Muhtasari wa Taarifa ya Awali ya Utekelezaji wa Mradi







*Kwa ajili ya Uhakiki kwa Kutumia Viwango vya Miradi ya Tabianchi, Jamii na Bionuwai (Climate, Community and Biodiversity (CCB) Project Standards)*

**MKUHUMI Unaotekelezwa na Jamii katika Misitu ya Pwani Tanzania**

**Taarifa ya awali ya utekelezaji wa mradi**

Kwa ajili ya Uhakiki kwa Kutumia Viwango vya Miradi ya Tabianchi, Jamii na Bionuwai

## 1) Utangulizi

Kitini hiki kinatoa muhtasari wa taarifa ya awali ya utekelezaji wa mradi unaojulikana kama 'MKUHUMI kwa ajili ya Jamii katika misitu ya pwani Tanzania kwa kuzingatia viwango vya miradi ya Tabianchi, Jamii na Bionuwai. Taarifa hii inaelezea maendeleo ya mradi katika kipindi cha kwanza cha utekelezaji ikihusiana na malengo ya jamii, tabianchi, na bionuwai.

*Muda wa uhakiki*


Kitini hiki kinatoa taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa kipindi cha kuanzia tarehe 21/4/2012 mpaka tarehe 30 na 20/4/2013

*Eneo la mradi*


Mradi upo katika Wilaya ya Lindi, Mkoa wa Lindi. Eneo la mradi linajumuisha vijiji 10: Kinyope, Kiwawa, Likwaya, Makumba, Milola Magharibi, Mkanga 1, Mkombamosi, Muungano, Nandambi na Ruhoma.

Eneo la mradi linajumuisha eneo la nyongeza la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika mashariki ambalo lina bionuwai nyingi

**Ramani ya 1.** Eneo la mradi.



**Ramani ya 2 vijiji vya mradi**




**Jedwali la 1: Tarehe muhimu zinaonyesha matukio ya utekelezaji wa mradi**

| Tarehe | Malengo makuu katika maendeleo ya utekelezaji wa mradi |
|---|---|
| Aprili – Mei 2010 | Mikutano ya kujitambulisha, shughuli za kuelimishana na kukubali mradi , mafunzo na kuanzisha kwa mfumo wa ufuatiliaji. |
| Juni – Septemba 2010 | Mikutano na wanavijiji katika ngazi ya vitongoji na vijiji kuhusu MKUHUMI. Wanavijiji kukubali kuendelea na mradi na TFCG na MJUMITA kuendelea na shughuli za utayari wa mradi. |
| Novemba 2011 – Februari 2013 | Malipo ya majaribio ya MKUHUMI yalifanyika kwa vijiji vilivyoshiriki katika mradi na kumaliza mchakato wa shughuli za mradi kama mipango ya matumizi bora ya ardhi na mipango ya usimamizi wa misitu. |
| 21 Aprili 2012 | Kuanza kwa kipindi cha mradi |
| Aprili 2013 | Kumalizika kwa kipindi cha kwanza cha utekelezaji wa mradi |
| Julai 2013 | Mipango ya usimamizi wa misitu na sheria ndogo; Mipango ya matumizi bora ya ardhi na sheria ndogo; Sheria ndogo za Mgawanyo wa mapato ya MKUHUMI ilipitishwa na kusainiwa na Halmashauri ya Wilaya. Mchakato wa kupitisha na kusaini ulichukuwa zaidi ya miaka miwili kutoka Julai 2011 hadi Julai 2013 wakati mipango mingi ilishapitishwa katika mikutano mikuu ya vijiji kati ya Julai hadi Desemba 2011 na kusainiwa katika ngazi ya Halmashauri mwezi Julai 2013. Kutokana na kwamba Halmashauri ya Wilaya ilipitisha zaidi ya siku 60 zinazoshauriwa katika mchakato wa kuoitisha mipango hii, wananvijiji walianza kutekeleza mipango yao na sheria ndogo mwaka 2012. Taarifa ya kina imetolewa katika sehemu ya CM 2.1 ya Taarifa ya Utekelezaji wa mradi |
| Mei – Juni 2013 | Makubaliano ya Utendaji yalifikiwa baina ya Jamii na |

| Tarehe | Malengo makuu katika maendeleo ya utekelezaji wa mradi |
|---|---|
| | MJUMITA na kusainiwa na wanavijiji yakukubali MJUMITA kuendelea na mchakato wa uthibitishaji kwa kutumia Viwango vya Hiari vya Kaboni (VCS) na Viwango vya Tabianchi, Jamii na bioanuwai. (CCB) |
| Machi 2014 | Awamu ya pili ya malipo ya MKUHUMI kwa vijiji vinavyoshiriki |

## 2) Tabianchi

### 3) CL1. Hali ya tabianchi kabla ya mradi


Tathmini ya hali tabianchi kabla ya mradi ilifanyika, na imebainika kuwa kilimo cha kuhama hama cha mazao ya biashara, mazao ya msimu na uchomaji wa mkaa ndiyo chanzo cha hali hiyo. Kabla ya mradi, maeneo ya misitu katika eneo la mradi yalikuwa hayana utaratibu wowote wa usimamamizi, maeneo hayo yangeweza kuingiliwa na kubadilishwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali bila kikwazo chochote. Maeneo ya misitu yaliweza kubadilishwa kuwa mashamba ya watu binafsi kwa kufyeka misitu. Kiwango cha ufyekaji kwa mwaka kilikuwa ni wastani wa asilimia 1.99 kuanzia mwaka 2001 hadi 2012.

Shughuli za mradi zilizofanyika ili kukabiliana na hali hiyo ni kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji ambapo wanakijiji walitenga asilimia 67 ya maeneo ya misitu kuwa misitu ya hifadhi za vijiji, misitu hiyo ni asilimia 75 ya misitu yenye hewa ukaa nyingi.Mradi pia ulihimiza kilimo hifadhi kwa kuboresha mbinu za kilimo na kuongeza uzalishaji wa mazao ili kupunguza mahitaji ya kufyeka misitu kwa ajili ya kilimo. Miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato imeanzishwa ikiwa ni pamoja na ufugaji wa nyuki vikundi vya kuweka na kukopa. Malipo yatakayotokana na mapato ya misitu na uuzaji wa hewa ukaa yatasaidia kupunguza gharama za utekelezaji wa MKUHUMI.

### CL2. Athari halisi chanya za Tabianchi

Katika kipindi cha utekelezaji wa mradi, ufyekaji wa misitu ulipungua kwa asilimia 29.4% ukilinganisha na hali ya awali ambapo jumla ya hekta 302 hazikufyekwa na kuzuia uzalishaji wa hewa ukaa kwa tani 40,178 kama inavyooneshwa kwenye ramani hapa chini.

**Ramani ya 3: Maeneo ya Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ukaa**



**Jedwali Na 2: kuonyesha kupungua kwa uzalishaji wa gesijoto (MKUHUMI) na kiwango cha hewa ukaa kwa ajili ya mauzo**

| Mwaka wa mradi | Mabadiliko ya hewa ukaa ya awali | Uzalishaji wa gesijoto wa awali | Madiliko ya hewa ukaa katika kipindi cha utekelezaji | Uzalishaji wa hewa ukaa katika kipindi cha utekelezaji | Uvujaji katika kipindi cha utekelezaji | Kiwango halisi cha kupunguza uzalishaji wa gesijoto | Kiwango cha hewa ya kuuza | Kiwango cha hewa ukaa cha akiba |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *Kwa mwaka* | *Kwa mwaka* | *Kwa mwaka* | *Kwa mwaka* | *Kwa mwaka* | *Kwa mwaka* | *Kwa mwaka* | *Kwa mwaka* |
| | $tCO_2$-e | $tCO_2$-e | $tCO_2$-e | $tCO_2$-e | $tCO_2$-e | $tCO_2$-e | $tCO_2$-e | $tCO_2$-e |
| 2012-2013 | (126,560) | 9,905 | (89,302) | 6,985 | - | 40,178 | 36,452 | 3,726 |

### CL3. Uvujaji

Katika kipindi cha utekelezaji wa mradi, hakukuwa na ongezeko la uharibifu na ufyekaji wa misitu katika ukanda wa uvujaji.

### CL4. Ufuatiliaji wa athari za tabiachi

Tathmini ya ufyekaji wa misitu ulifanyika, na matokeo yake yaliwasilishwa kwa kila kijiji kinachotekeleza mradi. Taarifa za sehemu ambayo ufyekaji umefanyika katika kila kijiji zilipatikana kwa kutumia wajumbe wa kamati za malisili wa kila kijiji ambao walibaini nani wanaohusika na kuhakikisha uharibifu haundelei.

## 4) Jamii

Yafuatayo ni malengo ya Jamii yaliyobainishwa na wadau ili kufikia faida nyingi za tabianchi, jamii na bionuwai.

Tabianchi

- Kupunguza uzalishaji wa gesijoto zinazotokana na ufyekaji wa misitu katika ardhi ya vijiji kwa kupitia usimamizi endelevu wa misitu.
- Kuongeza kiwango cha hewa ukaa katika misitu ya hifadhi ya vijiji kwa kuendeleza ukuaji wa asili wa misitu.

Jamii

- Kudumisha huduma za mfumo ikolojia wa msitu na upatikaji endelevu wa mazao ya misitu kupitia usimamizi shirikishi wa misitu ulio madhubuti na wenye usawa.
- Kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja kutokana na MKUHUMI kwa kuwekeza katika shughuli za kilimo bora na shughuli nyingine za kiuchumi kwa kuboresha hali ya ujumla ya maisha na kulenga zaidi kaya maskini na akina mama.
- Kuongeza ubora na upatikanaji wa huduma za jamii na miundombinu.

Bionuwai

- Kuhifadhi aina za viumbe vilivyo katika tishio na hatari ya kutoweka.
- Kuhifadhi eneo la nyongeza la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

Hili kufikia malengo haya, mradi unajihusisha na utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazofanana

#### 2.1 Athari zinazotegemewa

Mradi umelenga kupata athari halisi chanya kwa jamii zitakazoshiriki. Athari chanya za kijamii zinazotegemewa ni kama zinavyoorodheshwa hapa chini.

**Athari ya Kijamii (CM) 1.** Misitu inayomilikiwa na jamii itasimamiwa kwa njia shirikishi, madhubuti na yenye usawa.
**Athari ya Kijamii (CM) 2.** Mazao ya misitu yataendelea kupatikana na kuwafikia wanajamii wote pamoja na kaya maskini kwa namna zilizokubalika kwa njia shirikishi.

**Athari ya Kijamii (CM) 3.** Vijiji vitaongozwa vizuri zaidi.
**Athari ya Kijamii (CM) 4.** Wanajamii watakuwa na mfumo salama wa umiliki wa ardhi.
**Athari ya Kijamii (CM) 5.** Vyanzo vya maji vitalindwa vizuri zaidi
**Athari ya Kijamii (CM) 6.** Mmomonyoko wa udongo utapungua
**Athari ya Kijamii (CM) 7.** Pato la mtu mmoja mmoja litaongezeka na vyanzo vya mapato vitaongezeka kwa kulipwa fedha za MKUHUMI.
**Athari ya Kijamii (CM) 8.** Wakulima wanawake na wanaume, ikiwa ni pamoja na wanaotoka katika kaya maskini, wataanza kutumia mbinu za kilimo bora chenye faida zaidi, endelevu na kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi na watawekeza katika shughuli nyingine za kiuchumi na/au mbinu za kuongeza thamani ya mazao.
**Athari ya Kijamii (CM) 9.** Mapato yanayotokana na MKUHUMI yatachangia kuimarisha huduma za jamii na miundombinu.
**Athari ya Kijamii (CM) 10.** Vijiji vitakuwa na majengo ya ofisi

## 2.2 Matokeo


**Athari ya Kijamii (CM)1.** Misitu inayomilikiwa na jamii itasimamiwa kwa njia shirikishi, madhubuti na yenye usawa

Eneo lililopendekezwa katika kipindi cha kwanza cha utekelezaji lilikua hekta 35,018 kwa kuzingatia shughuli za awali kabla ya kuanza rasmi utekekezaji wa MKUHUMI ulinaotekelezwa na Shirika la Kuhifadhi misitu ya asili Tanzania ( TFCG) na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania ( MJUMITA) katika kipindi cha mwaka 2010-2012. Eneo lote lililopitishwa mwezi wa tano, 2013 lilikua hekta 33,726. Angalia jedwali namba 1

**Jedwali Na. 3.** Msitu wa hifadhi wa kijiji katika eneo la ardhi ya Kijiji kwa kila kijiji , mwezi wa tisa 2013

| **Kijiji** | **Eneo la ardhi ya kijiji lililopendekezwa kama msitu wa hifadhi wa Kijiji mwezi wanne 2012 ( ha)** | **Msitu wa hifadhi wa Kijiji katika eneo la ardhi ya kijiji mwezi wa tano 2013 (hekta)** |
|---|---:|---:|
| Kinyope | 1,861.10 | 2,016 |
| Kiwawa | 8,637.92 | 8,353 |
| Likwaya | 1,015.21 | 1,015 |
| Makumba | 3,141.63 | 2,636 |
| Milola Magharibi | 1,550.41 | 1,550 |
| Mkanga 1 | 1,541.50 | 1,548 |
| Mkombamosi | 4,114.83 | 3,237 |
| Muungano | 4,614.17 | 4,614 |
| Nandambi | 5,694.70 | 5695 |
| Ruhoma | 2,847.06 | 3062 |
| **Jumla kwa eneo lote la mradi** | **35,018.53** | **33,726.00** |

**Ramani ya 2.** Misitu ya hifadhi ya Kijiji mahali ilipo katika eneo la mradi




***Kiashiria CM 1.2 Eneo la misitu ya hifadhi ya vijiji lililotengwa kwa ajili ya usimamizi endelevu ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mazao ya misitu yasiyo mbao.***

Eneo la msitu wa hifadhi wa kijiji lililopo kwa matumizi endelevu kwa kijiji ni sawasawa na jumla ya eneo lote la msitu wa hifadhi wa Kijiji kama inavyoonyesha kwenye jedwali namba 1. Sheria ndogo za usimamizi wa misitu ya jamii imetofautisha aina tatu za matumizi ya misitu.

1) Matumizi ya msitu ambayo hayaitaji kibali kwa wakazi wa Kijiji
2) Matumizi ya msitu ambayo yanahitaji kibali cha bure kwa wakazi wa kijiji
3) Matumizi ya msitu yaliozuiliwa

***Kiashiria CM 1.3 Idadi ya vijiji vilivyo na kamati za maliasili***

Vijiji vyote 10 mpaka sasa vina kamati ya maliasili. Kamati hizi zina jukumu kubwa la kusimamia rasilimali zote za misitu kijijini pamoja na msitu wa hifadhi wa Kijiji.

***Kiashiria CM 1.4 Asilimia ya wanawake kwenye kamati ya maliasili kwa kila kijiji***

Hadi mwezi wa 9, 2013, wanawake kwenye kamati ya maliasili walikua kati ya asilimia 25 hadi 55 isipokua Kijiji kimoja cha Muungano ampapo wanawake kwenye kamati walikua pungufufu ya asilimia 33

**Jedwali namba 4.** Asilimia ya wajumbe wanawake katika kamati ya Maliasili, mwezi wa tisa 2013.

| Kijiji | Wanaume katika kamati | Wanawake katika kamati | Jumla ya wajumbe katika kamati Maliasili | Asilimia ya wajumbe wanawake katika kamati ya Maliasili |
|---|---|---|---|---|
| Kinyope | 8 | 4 | 12 | 33 |
| Kiwawa | 8 | 4 | 12 | 33 |
| Likwaya | 8 | 4 | 12 | 33 |
| Makumba | 5 | 6 | 11 | 55 |
| Milola mag | 8 | 4 | 12 | 33 |
| Mkanga 1 | 8 | 4 | 12 | 33 |

| Kijiji | Wanaume katika kamati | Wanawake katika kamati | Jumla ya wajumbe katika kamati Maliasili | Asilimia ya wajumbe wanawake katika kamati ya Maliasili |
|---|---|---|---|---|
| Mkombamosi | 8 | 4 | 12 | 33 |
| Muungano | 9 | 3 | 12 | 25 |
| Nandambi | 4 | 4 | 8 | 50 |
| Ruhoma | 7 | 5 | 12 | 42 |

***Kiashiria CM 1.5 Kiwango cha uharibifu wa misitu kwa kila kijiji katika msitu wa hifadhi wa kijiji.***
**Angalia jedwali namba 17**

***Kiashiria CM 1.6 Kiwango halisi cha mabadiliko ya hewa ukaa katika msitu wa hifadhi wa kijiji***
Kuna upungufu halisi wa kiasi cha hewa ukaa katika hifadhi za vijiji kwa kiasi cha hewa ukaa sawa sawa na tani za 40,

**Athari ya Kijamii (CM) 2.** Mazao ya misitu yataendelea kupatikana na kuwafikia wanajamii wote pamoja na kaya maskini kwa namna zilizokubalika kwa njia shirikishi

***Kiashiria CM 2.1 Idadi ya watu wenye haki ya kupata rasilimali za misitu ikiwa ni pamoja na kinga zilizowekwa kulinda haki za kaya masikini kuendelea kupata rasilimali za misitu.***
Katika vijiji vyote kila mwanajamii ana haki sawa ya kupata na kutumia mazao ya misitu na hii ikijumuisha wanawake wote na wanaume waliosajiliwa kama wakazi wa kijiji kwa mujibu wa sheria ndogo za msitu wa hifadhi wa kijiji.

**Athari ya Kijamii (CM) 3.** Vijiji vitaongozwa vizuri zaidi.

***Kiashiria CM 3.1 Idadi ya mikutano ya Halmashauri ya Kijiji iliyofanyika kwa mwaka katika kila kijiji.***

Idadi ya mikutano ya halmashauri ya kijiji iliyofanyika kwa mwaka kuanzia tarehe 1/4/2012 hadi tarehe 1/4/2013 ipo kati ya 2 hadi 12. Kwa kawaida vijiji vinatakiwa kufanya mkutano mmoja wa halmashauri ya kijiji kwa mwezi kwa maana kwamba ni mikutano 12 kwa mwaka kwa kijiji.

**Jedwali namba 5**. Idadi ya mikutano ya halmashauri ya kijiji iliyofanyika kuanzia mwezi Aprili, 2012 hadi mwezi Aprili, 2013

| Kijiji | Mikutano ya Halmashauri ya kijiji |
|---|---|
| Kinyope | 10 |
| Kiwawa | 8 |
| Likwaya | 5 |
| Makumba | 11 |
| Milola Magharibi | 10 |
| Mkanga 1 | 9 |
| Mkombamosi | 2 |
| Muungano | 5 |
| Nandambi | 10 |
| Ruhoma | 12 |

***Kiashiria CM 3.2 Idadi ya mikutano ya kamati ya matumizi bora ya ardhi kwa mwaka kwa kila kijiji***
Kwa kawaida kamati ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji inatakiwa kufanya mkutano mmoja kwa mwezi na hii inamaanisha ni sawa na mikutano 12 kwa mwaka kwa Kijiji

***Jedwali Na.6 Idadi ya mikutano ya kamati ya matumizi bora ya ardhi kwa mwaka kwa kila kijiji***

| Kijiji | Mikutano ya kamati ya matumizi bora ya ardhi kwa mwaka |
|---|---|
| Kinyope | 6 |
| Kiwawa | 4 |
| Likwaya | 15 |
| Makumba | 7 |
| Milola Magharibi | 8 |
| Mkanga 1 | 11 |
| Mkombamosi | 7 |
| Muungano | 9 |
| Nandambi | 8 |
| Ruhoma | |

***Kiashiria CM 3.3 Idadi ya mikutano ya hadhara ya kijiji iliyofanyika kwa mwaka katika kila kijiji***

Mikutano ya hadhara ya kijiji inafanyika kwa kuhusisha wakazi wote wa kijiji wanawake kwa wanaume. Mikutano hii inatakiwa kufanyika mara moja kwa kila baada ya miezi mitatu yaani mara nne kwa mwaka kwa kijiji.

***Jedwali Na.7: Idadi ya mikutano ya hadhara ya kijiji iliyofanyika kwa mwaka katika kila kijiji***

| Kijiji | Idadi ya Mikutano ya hadhara kuanzia mwezi Aprili, 2012 hadi mwezi Aprili, 2013 |
|---|---|
| Kinyope | 2 |
| Kiwawa | 2 |
| Likwaya | 1 |
| Makumba | 3 |
| Milola Magharibi | 3 |
| Mkanga 1 | 3 |
| Mkombamosi | 4 |
| Muungano | 1 |
| Nandambi | 3 |
| Ruhoma | 4 |

***Kiashiria CM 3.4 Asilimia ya wajumbe wanawake katika halmashauri ya kijiji.***

Hadi mwezi Septemba, 2013 wajumbe wanawake katika Halmashauri ya kijiji walikua kati ya asilimia 17 hadi 35

**Jedwali Na 8. Mgawanyo wa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kuzingatia jinsia kwa kila kijiji**

| Kijiji | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia ya wajumbe wanawake katika Halmashauri ya Kijiji |
|---|---|---|---|---|
| Kinyope | 12 | 5 | 17 | 29.4 |
| Kiwawa | 17 | 5 | 22 | 22.7 |
| Likwaya | 18 | 6 | 24 | 25 |
| Makumba | 14 | 3 | 17 | 17.9 |
| Milola Magharibi | 13 | 5 | 18 | 27.8 |
| Mkanga 1 | 19 | 6 | 25 | 24.0 |
| Mkombamosi | 19 | 6 | 25 | 24.0 |
| Muungano | 20 | 5 | 25 | 20.0 |
| Nandambi | 18 | 7 | 25 | 28.0 |
| Ruhoma | 13 | 7 | 20 | 35.0 |

**Athari ya Kijamii (CM) 4. Wanajamii watakuwa na mfumo salama wa umiliki wa ardhi**

***Kiashiria CM 4.1 Idadi ya vijiji vyenye vyeti vya ardhi ya kijiji***
Katika vijiji vyote 10 vya mradi , hakuna hata kijiji kimoja chenye cheti cha ardhi ya Kijiji kilichosainiwa na kamishna wa ardhi katika ofisi ya Kijiji. Mpaka sasa marekebisho ya mipaka ya vijiji vyote yamepelekwa katika ngazi ya halmashauri ya wilaya kwa ajili ya taratibu zingine za kumalizia kupitisha marekebisho ya mipaka hiyo. Kwa kawaida Kijiji hakiwezi kupata cheti cha ardhi ya Kijiji kama mipaka yake haijakubalika na kupitishwa kisheria.

***Kiashiria CM 4.2 Idadi ya vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi na sheria ndogo za mipango ya matumizi bora ya ardhi***

Vijiji vyote mpaka sasa vina mipango ya matumizi bora ya ardhi. Mipango hii imepitishwa na kusainiwa katika ngazi ya Wilaya na nakala zimerudisha katika vijiji vyote 10.

***Kiashiria CM 4.3 Idadi ya vijiji vyenye masjala ya ardhi ya vijiji***
Vijiji vyote vina makabati maalumu ya chuma ya kuifadhia nyaraka za usajili wa ardhi. Hata hivyo hakuna hata kijiji kilichopatiwa vitabu vya kusajili hati za kimila mpaka sasa wala kumbukumbu ya ardhi iliyosajiliwa kwa mtu yeyote. .

**Athari ya Kijamii ( CM) 5. Vyanzo vya maji vitalindwa vizuri zaidi**
***Kiashiria CM 5.1 Idadi ya vijiji vyenye vyanzo vya maji katika misitu ya hifadhi ya vijiji***
Vijiji vingi vya mradi vinategemea vyanzo vya maji ambavyo vipo juu ya ardhi ikiwemo vijito vidogo vidogo, mabwawa na chemchem kwa matumizi ya nyumbani na kwa ajili ya shughuli za kilimo. Kuwepo kwa hifadhi ya misitu ya vijiji hivi kwa sasa kunachangia kuhifadhi vyanzo vya maji na hivyo vyanzo hivi vina hesabika kuwa vimelindwa ipasavyo

**Athari ya Kijamii ( CM) 6. Mmomonyoko wa udongo utapungua**
***Kiashiria CM 6.1 Idadi ya vijiji vyenye miinuko mikali katika misitu ya hifadhi ya vijiji.***
Vijiji 7 vimetenga misitu ya hifadhi ya kijiji katika miinuko mikali inayozidi nyuzi 20 (20°) . Vijiji hivyo ni Muungano, Kiwawa, Nandambi, Ruhoma, Milola Magharibi, Mkombamosi and Makumba.

***Kiashiria CM 6.2 Idadi ya vijiji vyenye wakulima wanaotekeleza mbinu za uhifadhi wa ardhi (udongo***)

Kwa kuzingatia mafunzo ya wakulima na mafunzo ya wakufunzi kilimo , wakulima wanaotumia mbinu bora za kilimo kwa kila kijiji ni kama inavyoonshesha hapo chini.
**Jedwali Na. 9:** ***Idadi ya vijiji vyenye wakulima wanaotekeleza mbinu za uhifadhi wa ardhi***

| Kijiji | Idadi ya wakulima wanautumia mbinu bora za uhifadhi wa ardhi (udongo) kwa kipindi cha cha mwezi wa 9, 2013 |
|---|---|
| Kinyope | Mafunzo ya Kilimo hifadhi bado hayajafanyika |
| Kiwawa | Mafunzo ya Kilimo hifadhi bado hayajafanyika |
| Likwaya | 6 |
| Makumba | Mafunzo ya Kilimo hifadhi bado hayajafanyika Training |
| Milola Magharibi | 16 |
| Mkanga | 10 |
| Mkombamosi | 14 |
| Muungano | 10 |
| Nandambi | 20 |
| Ruhoma | 21 |
| **Jumla** | **97** |

**Athari ya Kijamii (CM) 7. Pato la mtu mmoja mmoja litaongezeka na vyanzo vya mapato vitaongezeka kwa kulipwa fedha za MKUHUMI**

***Kiashiria CM 7.1 Jumla ya malipo ya fedha za MKUHUMI zilizolipwa kwa kila kijiji ikijumuisha malipo kwa kila mtu na michango ya miradi ya maendeleo***.

Jumla ya kiasi cha shilingi 284,842,940 zililipwa kwa vijiji kumi, na malipo yalianzia kiasi cha shilingi 4,647,200 hadi shilingi 51,511,200. Malipo hayo yalifanyika kuanzia mwezi wa 11, 2011 hadi mwezi wa 7, 2013.

**Jedwali Namba 10.** Muhtasari wa malipo yote kwa wanaume, wanawake pamoja na watoto kwa kila Kijiji.

| Kijiji | Wanaume | Wanawake | Watoto na wategemezi | Jumla | Jumla ya pesa zote zilizolipwa (Shilingi za kitanzania) |
|---|---|---|---|---|---|
| Kinyope | 963 | 1,348 | 1,596 | 3,907 | 12,648,900 |
| Kiwawa | 379 | 441 | 918 | 1,738 | 49,143,000 |
| Likwaya | 131 | 167 | 263 | 561 | 7,268,086 |
| Makumba | 172 | 217 | 281 | 670 | 48,256,800 |
| Milola Magharibi | 507 | 541 | 1,351 | 2,399 | 4,647,200 |
| Mkanga | 196 | 231 | 353 | 780 | 8,375,794 |
| Mkombamosi | 118 | 639 | 1,508 | 2,265 | 32,268,000 |
| Muungano | 507 | 541 | 1,351 | 2,399 | 51,511,200 |
| Nandambi | 200 | 236 | 295 | 731 | 49,642,000 |
| Ruhoma | 133 | 213 | 255 | 601 | 21,081,960 |
| **Total** | **3,306** | **4,574** | **8,171** | **16,051** | **284,842,940** |

***Kiashiria CM 7.2 Jumla ya malipo ya fedha za MKUHUMi zilizolipwa kwa kila mtu katika kila Kijiji***.

Jumla ya kiasi cha shilingi 199,598,000 zimelipwa kwa kila mtu kuanzia kiasi cha shilingi 38,384,000 hadi shilingi sifuri ( 0) kwa kijiji.

**Jedwali namba 11.** Malipo ya fedha za MKUHUMI kwa wanajamii na michango ya miradi ya maendeleo ya jamii

| Kijiji | Miradi ya maendeleo | Kiasi cha pesa kilicholipwa kwa wanajamii | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kinyope | 12,648,900 | - | 12,648,900 |
| Kiwawa | 5,693,000 | 43,450,000 | 49,143,000 |
| Likwaya | 536,086 | 6,732,000 | 7,268,086 |
| Makumba | 14,806,800 | 33,450,000 | 48,256,800 |
| Milola Magharibi | 4,647,200 | - | 4,647,200 |
| Mkanga 1 | 3,695,794 | 4,680,000 | 8,375,794 |
| Mkombamosi | 7,353,000 | 24,915,000 | 32,268,000 |
| Muungano | 13,127,200 | 38,384,000 | 51,511,200 |
| Nandambi | 20,402,000 | 29,240,000 | 49,642,000 |
| Ruhoma | 2,334,960 | 18,747,000 | 21,081,960 |
| **Total** | **85,244,940** | **199,598,000** | **284,842,940** |

Makadirio ya kiwango cha kubadilisha pesa: Dola 1 sawa na Shilingi ya Tanzania 1560

***Kiashiria CM 7.3 Jumla ya kiasi cha malipo ambacho wanakijiji wametenga kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jamii katika kila kijiji***

**Jedwali namba 12**. Kiasi cha pesa kilichotengwa na jamii kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutokana na mgawanyo wa mapato ya kila mwanakijiji

| **Mradi** | **Kinyope** | **Kiwawa** | **Likwaya** | **Makumba** | **Milola Magharibi** | **Mkanga** | **Mkombamosi** | **Muungano** | **Nandambi** | **Ruhoma** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi au ukarabati wa huduma za afya kama vile zahanati | 5,216,300 | | | | | 3,678,794 | | | 19,242,000 | |
| Ujenzi wa ofisi ya kijiji | 3,216,300 | 3,410,000 | | 3,482,000 | 4,447,200 | | 4,190,000 | 4,200,000 | | 474960 |
| Ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu au vyoo vya shule | 3,216,300 | | | 9,126,000 | | | | 6,116,000 | | |
| Ununuzi wa madawati kwa shule ya msingi | | | | 115,000 | | | 1,450,000 | 1,000,000 | | 360,000 |
| Michango kwa ajili ya ujenzi wa msikiti | | | | 500,000 | | | | | | |
| Michango kwa ajili ya kuboresha huduma za maji majumbani | | | 536,086 | | | | | | | |
| Michango kwa ajili ya gharama za kamati za maliasili | 1,000,000 | 1,725,000 | | 1,068,800 | 200,000 | 17,000 | 1,233,000 | 1,471,200 | 500,000 | 700,000 |
| Michango kwa ajili ya kamati maalumu ya MKUHUMI | | 558,000 | | 465,000 | | | 480,000 | 340,000 | 300,000 | |
| Ununuzi wa trekta dogo (power tiller) | | | | | | | | | | 450,000 |
| Ununuzi wa nyavu ya kusakia wanyawa mashambani ili kuzuia upotevu wa mazao | | | | | | | | | | 350,000 |
| Ununuzi wa viti kwa ajili ya ofisi ya kijiji | | | | | | | | | 360,000 | |
| **Jumla** | **12,648,900** | **5,693,000** | **536,086** | **14,756,800** | **4,647,200** | **3,695,794** | **7,353,000** | **13,127,200** | **20,402,000** | **2,334,960** |

***Kiashiria CM 7.4 Idadi ya wanawake waliopokea fedha zinazotokana na MKUHUMI.***
Wanawake 4574 walipokea fedha . Angalia Jedwali namba 8 kwa ufafanuzi zaidi

***Kiashiria CM 7.5 Idadi ya wanaume waliopokea fedha zinazotokana na MKUHUMI***
Wanaume 3306 walipokea fedha. Angalia jedwali namba 8 kwa ufafanuzi zaidi

***Kiashiria CM 7.6 Idadi ya watoto na wategemezi waliopokea fedha zinazotokana na MKUHUMI***
Watoto na wategemezi 8171 walitengewa malipo yaliyofanyika kwa mama au mlezi teule. Angalia jedwali namba 8 kwa ufafanuzi zaidi.

***Kiashiria CM 7.7 Idadi, aina na thamani ya miradi ya maendeleo iliyokamilika inayogharamiwa na fedha zinazotokana na MKUHUMI.***
Wanajamii walichagua kuwekeza katika miradi 17 ya maendeleo ambayo bado inaendelea au imeshakamilika. Kwa baadhi ya miradi siyo pesa pekee itokanayo na MKUHUMI imekua kama chanzo cha pesa kwa miradi hiyo.

***Kiashiria CM 7.8 Kiwango cha dhahabu: Angalau asilimia 50 ya kaya zilizo katika kiwango cha chini kabisa cha hali ya maisha wanaweza kunufaika kwa kiwango kikubwa kupitia mradi wa MKUHUMI.***

**Jedwali namba 11.** Idadi na aina ya miradi ya maendeleo inayogharamiwa na fedha zitokanazo na MKUHUMI .

| **Kijiji** | **Idadi ya miradi ya maendeleo kwa Kijiji** | **Aina ya Miradi ya maendeleo** | **Hali halisi hadi mwezi wa tisa 2013** |
|---|---|---|---|
| Kinyope | 3 | Ujenzi wa Zahanati | Ujenzi unaendelea |
| | | Ujenzi wa ofisi ya Kijiji | Ujenzi umekamilika na jengo linatumika |
| | | Ujenzi wa vyoo vya shule ya msingi kwa kutumia matofali ya simenti | Ujenzi umekamilika na vyoo vinatumika |
| Kiwawa | 1 | Ofisi ya Kijiji | Ujenzi umekamilika na jengo linatumika |
| Likwaya | 1 | Ukarabati wa chanzo cha maji (kisima) kwa ajili ya matumizi ya nyumbani) | Ukarabati umekamililka na kisima kinatumika |
| Makumba | 4 | Ofisi ya Kijiji | Ujenzi umekamilika na jengo linatumika |
| | | Ujenzi shule ya msingi | Ujenzi unaendelea |
| | | Madawati kwa shule ya msingi | Mradi umekalika |
| | | Ukarabati wa msikiti wa Kijiji | Ujenzi upo katika hatua za awalo |
| Milola Magharibi | 1 | Ujenzi wa ofisi ya Kijiji | Ujenzi umekamilika na jengo linatumika |
| Mkanga 1 | 1 | Ujenzi wa Zahanati | Ujenzi unaendelea na bado upo katika hatua ya msingi |
| Mkombamosi | 2 | Ujenzi wa ofisi | Ujenzi umekamilika na jengo linatumika |
| | | Madawati ya shule ya msingi | Mradi umekamilika |
| Muungano | 1 | Vyumba viwili vya madarasa ya shule ya msingi katika kitongoji cha uleka | Ujenzi unaendelea na upo katika hatua ya kupaua |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Nandambi | 1 | Ujenzi wa Zahanati | Ujenzi unaendelea na upo katika hatua ya kupaua |
| Ruhoma | 2 | Power tiller | Mradi umekamilika |
| | | Ujenzi wa ofisi ya Kijiji | Ujenzi umekamilika na jengo linatumika |
| | | Nyavu za kukamatia wanyama waharibifu | Zilinunuliwa na zinatumika |
| | **17** | | |

***Miradi ya maendeleo katika kijiji cha kinyope***

Picha namba 1. Choo cha shule ya msingi kilichojengwa kwa fedha zilizotokana na malipo ya utekelezaji wa MKUHUMI.



Picha namba 2. Ujenzi wa Zahanati unaendelea katika kijiji cha Kinyope mwezi wa 9, 2013



***Miradi ya maendeleo katika kijiji cha Makumba***

Picha namba 3. Chumba cha darasa kwa wanafunzi wa darasa la 3 na 4 katika shule ya msingi Makumba na nyumba ya walimu



***Miradi ya maendeleo katika kijiji cha Muungano***

Picha ya 4. Vyumba viwili vipya vya madarasa ya shule ya msingi katika kitongoji cha Uleka



***Miradi ya maendeleo katika kijiji cha Nandambi***

Picha namba 5. Ujenzi wa jengo la zahanati unaoendelea katika kijiji cha Nandambi



**Athari ya kijamii (CM 8). Wakulima wanawake na wanaume, ikiwa ni pamoja na wanaotoka katika kaya maskini, wataanza kutumia mbinu za kilimo bora chenye faida zaidi, endelevu na kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi na watawekeza katika shughuli nyingine za kiuchumi na/au mbinu za kuongeza thamani.**

***Kiashiria CM 8.1 Idadi ya wanawake na wanaume waliopokea mafunzo kuhusu mbinu bora za kilimo, mbinu za kuongeza thamani ya mazao na shughuli nyingine za kiuchumi katika eneo la mradi na vijiji vilivyo katika ukanda wa uvujaji***

Mradi umesaidia aina tatu za miradi ya maendeleo ambayo imelenga kuboresha maisha ya wanajamii, miradi hiyo ni kilimo bora, uanzishwaji wa taasisi ndogo za kifedha na ufugaji wa nyuki .

**Jedwali namba 10.** Idadi na aina ya miradi ya maendeleo ya kujiongezea ili kuboresha maisha iliyoanzishwa kwa kijiji na idadi ya watu walionufaika.

| **Kijiji** | **Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo ya mbinu bora za kilimo** | **Idadi ya watu waliopatiwa mfaunzo ya mikopo midogomidogo (Mfumo wa Hisa) ,** | **Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki** | **Jumla ya watu waliopatiwa mafunzo** | **Idadi ya miradi iliyoanzishwa** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kinyope | Bado | 3 | 28 | 31 | 2 |
| Kiwawa | Bado | 5 | 30 | 35 | 2 |
| Likwaya | 18 | 3 | 26 | 47 | 3 |
| Makumba | Bado | 10 | 30 | 40 | 2 |
| Milola Magharibi | 24 | 4 | 29 | 57 | 3 |
| Mkanga 1 | 20 | 5 | 28 | 53 | 3 |
| Mkombamosi | 17 | 10 | 0 | 27 | 2 |
| Muungano | 17 | 8 | 25 | 50 | 3 |

| **Kijiji** | **Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo ya mbinu bora za kilimo** | **Idadi ya watu waliopatiwa mfaunzo ya mikopo midogomidogo (Mfumo wa Hisa) ,** | **Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki** | **Jumla ya watu waliopatiwa mafunzo** | **Idadi ya miradi iliyoanzishwa** |
|---|---|---|---|---|---|
| Nandambi | 32 | 4 | 27 | 63 | 3 |
| Ruhoma | 21 | 3 | 26 | 50 | 3 |
| **Jumla** | **149** | **55** | **249** | **453** | |

***Kilimo bora***

Mradi uliandaa mkakati wa utekelezaji wa kilimo ambao ulilenga kuboresha hali za maisha ya wanajamii, kupunguza ufyekaji wa misitu unaosababishwa na kilimo cha kuhamahama na kuboresha hali inayohimili mabadiliko ya tabia nchi.

Pia mradi ulitoa mafunzo ya siku 5 yaliyofanyika kwa nadharia na vitendo kwa wakufunzi 18 wa kilimo kutoka katika vijiji saba.

**Jedwali namba 11.** Idadi ya wakufunzi jamii kilimo waliopatiwa mafunzo na mradi

| **Kijiji** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Kinyope | 0 | 0 | 0 |
| Kiwawa | 0 | 0 | 0 |
| Likwaya | 1 | 1 | 2 |
| Makumba | 0 | 0 | 0 |
| Milola Magharibi | 1 | 3 | 4 |
| Mkanga1 | 1 | 1 | 2 |
| Mkombamosi | 0 | 2 | 2 |
| Muungano | 0 | 2 | 2 |
| Nandambi | 2 | 2 | 4 |
| Ruhoma | 1 | 1 | 2 |
| **Jumla** | **6** | **12** | **18** |

Katika vijiji 7 (yenye vitongoji 9) mradi umetoa mafunzo ya Kilimo hifadhi kwa wanawake 54 na wanaume 95.

**Jedwali namba 12.** Idadi ya wanawake na wanaume waliopatiwa mafunzo na mradi kuhusiana na mbinu bora za kilimo

| **Village** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Kinyope | 0 | 0 | 0 |
| Kiwawa | 0 | 0 | 0 |
| Likwaya | 6 | 12 | 18 |
| Makumba | 0 | 0 | 0 |
| Milola Magharibi | 7 | 17 | 24 |
| Mkanga1 | 5 | 15 | 20 |
| Mkombamosi | 7 | 10 | 17 |
| Muungano | 7 | 10 | 17 |
| Nandambi | 14 | 18 | 32 |
| Ruhoma | 8 | 13 | 21 |
| **Jumla** | **95** | **54** | **149** |



Mafunzo ya kilimo hifadhi kwa nadharia  katika kitongoji cha  Kilombwani Kijiji cha Nandambi



Mafunzo ya kilimo hifadhi  kwa vitendo  (hatua ya uchimbaji mashimo) katika Kijiji cha Likwaya



Wanakikundi cha kilimo  hifadhi wakiwa tayari kuanza uvunaji wa mahindi katika kijiji cha Ruhoma.



Uvunaji wa Mahindi katika Kijiji cha  Ruhoma

***Taasisi ndogo za Kifedha***

Mradi umetoa mafunzo ya vikundi vya kuweka na kukopa ( vikundi vya hisa) katika vijiji vyote 10 ikihusisha wanawake 20 na wanaume 35

**Jedwali namba  13.** Idadi ya wakufunzi  wanaume na wanawake waliopatiwa mafunzo ya kusaidia vikundi vya hisa ( (kuweka na kukopa) kijijini

| Kijiji | Wanawake | Wanaume | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kinyope | 0 | 3 | 3 |
| Kiwawa | 0 | 5 | 5 |
| Likwaya | 2 | 1 | 3 |
| Makumba | 6 | 4 | 10 |
| Milola Magharibi | 4 | 0 | 4 |
| Mkanga1 | 0 | 5 | 5 |
| Mkombamosi | 4 | 6 | 10 |
| Muungano | 2 | 6 | 8 |
| Nandambi | 1 | 3 | 4 |
| Ruhoma | 1 | 2 | 3 |
| **Jumla** | **20** | **35** | **55** |

***Ufugaji wa Nyuki***

Mradi umetoa mafunzo ya ufugaji wa nyuki kwa jumla ya wanaume 177 na wanawake 96 na umegawa mizinga ya kisasa ipatayo 228.

**Jedwali namba 14.** Idadi ya wanawake na wanaume waliopatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki na idadi ya mizinga iliyotolewa

| **Kijiji** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Idadi ya mizinga iliyotolewa** |
|---|---|---|---|
| Kinyope | 15 | 13 | 21 |
| Kiwawa | 19 | 11 | 20 |
| Likandilo | 14 | 10 | 20 |
| Likwaya | 13 | 13 | 21 |
| Makumba | 20 | 10 | 20 |
| Milola Magharibi | 25 | 4 | 21 |
| Mkanga 1 | 16 | 12 | 21 |
| Mkombamosi | 11 | 2 | 21 |
| Muungano | 11 | 2 | 21 |
| Nandambi | 15 | 12 | 21 |
| Ruhoma | 19 | 7 | 21 |
| **Total** | **177** | **96** | **228** |

***Indicator CM 8.2 Idadi ya wakulima wanawake na wanaume wanaotumia mbinu mpya za kilimo, mbinu za kuongeza thamani ya mazao na shughuli nyingine za kiuchumi katika eneo la mradi na vijiji vilivyo katika ukanda wa uvujaji***.

Kwa kuzingatia takwaimu zilizotolewa na wakulima 97( kati ya 149 waliopatiwa mafunzo) ambao wameiga na kutekeleza kilimo hifadhi karibia ekari 30, wastani wa mavuno ya mahindi kwa ekari ulikua ni kilo 484 ukilinganisha na kilo 350 kwenye shamba la kilimo cha mazoea (kawaida) na hii ni sawa na ongezeko la mavuno kwa asilimia 38

**Jedwali namba 15.** Idadi ya wakulima walioiga na kutekeleza mbinu bora za kilimo.

| **Kijiji** | **Idadi ya wakulima walioiga na kutekeleza kilimo hifadhi mwezi 6, 2013** |
|---|---|
| Kinyope | Mafunzo ya kilimo hifadhi bado hayajafanyika |
| Kiwawa | Mafunzo ya kilimo hifadhi bado hayajafanyika |
| Likwaya | 6 |
| Makumba | Mafunzo ya kilimo hifadhi bado hayajafanyika |
| Milola Magharibi | 16 |
| Mkanga | 10 |
| Mkombamosi | 14 |
| Muungano | 10 |
| Nandambi | 20 |
| Ruhoma | 21 |
| **Jumla** | **97** |

***Kiashiria CM 8.3 Kiwango cha dhahabu: Mradi upo katika ukanda wa nchi yenye kiwango cha chini cha maendeleo***

Kwa mujibu wa taarifa ya mwaka 2013 ya Shirika la programu la maendeleo la umoja wa mataifa ( UNDP), nchi ya Tanzania imetajwa kama ni nchi yenye kiwango cha chini cha maendeleo

**Athari ya Kijamii (CM) 9. Mapato yanayotokana na MKUHUMI yatachangia kuimarisha huduma za jamii na miundombinu**

***Kiashiria  CM 9.1 Mabadiliko katika huduma za jamii zilizopo kijijini (shule za msingi, zahanati, sehemu za mikutano, ofisi za vijiji, upatikanaji wa maji) na miundombinu ya barabara (idadi na ubora wa barabara)***

Kwa kupitia mradi huduma nyingi za jamii kwa sasa zinapatikana, vijiji vyote kwa sasa vina ofisi za vijiji, kwa vijiji vitatu vya Makumba, Muungano na Kinyope huduma za jamii zinaendelea kuboreshwa na huduma nyingine zimekamilika katika majengo ya shule za msingi  ikiwa ni pamoja na vyumba vya madarasa , ofisi ya walimu na ujenzi wa matundu ya vyoo. Aidha kwa vijiji vitatu vya Nandambi, Kinyope na Mkanga 1 uboreshaji wa huduma za afya unaendelea hasa kwa upande wa ujenzi wa Zahanati

**Athari ya Kijamii (CM) 10. Vijiji vitakuwa na majengo ya**

***Kiashiria CM 10.1 Idadi ya vijiji vyenye ofisi za tofali na kuezekwa kwa bati  na zinazofanya kazi***
Kwa msaada wa  mradi wa MKUHUMI, vijiji vyote kumi vimejenga ofisi za vijiji

## 5) Bionuwai

Mradi wa  'MKUHUMI Unaotekelezwa na Jamii katika Misitu ya Pwani Tanzania' una malengo mawili yanayohusiana na thamani za bionuwai katika eneo la mradi.

Lengo la 1. Kuhifadhi aina za viumbe vilivyo katika tishio na hatari ya kutoweka.
Lengo la 2. Kuhifadhi eneo la nyongeza la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

**Athari za bionuwai B 1. Idadi ya viumbe vilivyo katika tishio na hatari ya kutoweka vinaendelea kuwepo katika eneo la mradi**

***Kiashiria  B 1.1 Uwepo wa komba wa Rondo ambao wapo katika hatari kubwa ya kutoweka katika eneo la mradi***.

Kati ya tarehe 2 hadi 6/9/2013, komba wa Rondo ambao wapo katika hatari kubwa ya kutoweka walionekana katika maeneo mawili ndani ya eneo la mradi.

***Kiashiria B 1.2 Uwepo wa aina tatu ya mimea iliyo hatarini kutoweka na aina nne ya mimea iliyo katika mazingira ya hatari ya kutoweka***

**Jedwali namba 16.** Hali halisi ya mimea iliyo hatarini na katika mazingira ya hatari kutoweka katika kipindi cha mwezi wa 9, 2013.

| **Jina la Kisayansi** | **Hali halisi kwa mujibu wa (IUCN 2011)** | **Imetambulika mwaka 2013 ndani ya eneo la mradi** | **Vijiji ambavyo mimea hiyo imetambulika** |
|---|---|---|---|
| *Leptactina papyrophloea* Verdc. | Hatari ya kutoweka | Ndio | Ruhoma, Muungano, Kiwawa |
| *Dichapetalum braunii* Engl. & K. Krause | Hatari ya kutoweka | Ndio | Mkanga 1 |
| *Pteleopsis apetala* Vollesen. | Hatari ya kutoweka | Ndio | Likandilo, Mkanga 1 |
| *Monanthotaxis trichantha* (Diels) Verdc. | Hatarini | Ndio | Ruhoma, Muungano, Likandilo, Mkombamosi |
| *Mimosops acutifolia* Mildbr. | Hatarini | Ndio | Mkombamosi, Muungano |
| *Peponium leucanthum* (Gilg) Cogn. | Hatarini | Ndio | Ruhoma, Muungano, Mkombamosi, Mkanga 1 |
| *Bauhinia loeseneriana* Harms. | Hatarini | Ndio | Ruhoma |
| *Cincinnobotrys pulchella* (Brenan) Jac.-Fel. | Coastal Forest Endemic | Hapana | |

**Athari ya Bionuwai ya 2. Eneo la nyongeza la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki kuendelea kuwepo katika eneo la mradi.**

***Kiashiria B 2.1 Hekta za misitu katika kila kijiji cha mradi***

**Jedwali namba 17.** Ene la msitu katika ardhi ya kijiji na eneo lililokuwa katika msitu wa hifadhi wa kijiji .

| Village | Eneo la msitu katika ardhi ya Kijiji, mwezi wa 4 2012 (hekta) | Eneo la msitu wa hifadhi wa Kijiji lililopendekezwa katika ardhi ya Kijiji, mwezi wa 4 2012 (hekta) | Eneo lililokua na msitu katika ardhi ya Kijiji, mwezi wa 4, 2013 ( hekta) | Eneo la msitu wa hifadhi wa kijiji lililopitishwa , mwezi wa 4, 2013 (hekta) |
|---|---:|---:|---:|---:|
| Kinyope | 2540 | 1,861.10 | 2,419 | 2,016 |
| Kiwawa | 11,136 | 8,637.92 | 11,038 | 8,353 |
| Likwaya | 1,323 | 1,015.21 | 1,302 | 1,015 |
| Makumba | 2,281 | 3,141.63 | 2,232 | 2,636 |
| Milola Magharibi | 2318 | 1,550.41 | 2,290 | 1,550 |
| Mkanga 1 | 2045 | 1,541.50 | 2,003 | 1,548 |
| Mkombamosi | 4026 | 4,114.83 | 3,982 | 3,237 |
| Muungano | 6539 | 4,614.17 | 6,431 | 4,614 |
| Nandambi | 6515 | 5,694.70 | 6,406 | 5695 |
| Ruhoma | 3200 | 2,847.06 | 3,169 | 3062 |
| **Jumla katika eneo la mradi** | **41,924** | **35,018.53** | **41,271** | **33,726.00** |

**Athari ya Bionuwai ya 3. Kuna msukumo mdogo wa ufyekaji wa misitu na uharibifu wa misitu katika eneo la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki.**

***Kiashiria B 3.1 Kiwango cha ufyekaji wa misitu na mtawanyiko kwenye maeneo yenye bionuwai nyingi***

Maeneo yenye bionuwai nyingi ni yale ya misitu ya hifadhi ya vijiji ambayo aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka wameonekana .

**Jedwali namba 18.** Kiwango cha ufyekaji wa misitu kwenye maeneo yenye bionuwai nyingi

| Kijiji | Wastani kwa mwaka wa Kiwango cha ufyekaji wa misitu kwa kijiji kati ya mwaka 2001 and 2012 | Kiwango cha ufyekaji wa misitu kwa mwaka kwa Kijiji katika kipindi cha utekelezaji wa mradi | Kiwango cha ufyekaji wa misitu ndani ya misitu ya hifadhi ya Kijiji wakati wa utekelezaji wa mradi |
|---|---:|---:|---:|
| Kinyope | 1.87% | 4.83% | 3.38% |
| Kiwawa | 1.27% | 0.87% | 0.74% |
| Likwaya | 4.7% | 1.78% | 0.12% |
| Makumba | 3% | 2.11% | 1.69% |
| Milola Magharibi | 2.49% | 1.2% | 1.57% |
| Mkanga 1 | 2.77% | 1.85% | 0.47% |
| Mkombamosi | 2.2% | 1.09% | 0.11% |
| Muungano | 2.1% | 1.53% | 1.07% |
| Nandambi | 1.46% | 1.75% | 0.92% |

| Kijiji | Wastani kwa mwaka wa Kiwango cha ufyekaji wa misitu kwa kijiji kati ya mwaka 2001 and 2012 | Kiwango cha ufyekaji wa misitu kwa mwaka kwa Kijiji katika kipindi cha utekelezaji wa mradi | Kiwango cha ufyekaji wa misitu ndani ya misitu ya hifadhi ya Kijiji wakati wa utekelezaji wa mradi |
|---|---|---|---|
| Ruhoma | 1.03% | 1.16% | 0.23% |
| **Jumla katika eneo la mradi** | | **1.58%** | 0.91% |

**Athari ya bionuwai ya 4: Jamii na wadau wanajihusisha kikamilifu katika usimamizi wa misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki katika eneo la mradi**

***Kiashiria B 4.1 Awamu za kufanya doria katika msitu wa hifadhi wa kijiji***.

Kwa kawaida kamati za maliasili za vijiji zinafanya doria mara moja kwa wiki na hii ni sawa na mara nne kwa mwezi kwa kila kijijiji. Doria hizi hufanyika katika misitu yote ya kijiji ikiwemo na misitu ya hifadhi ya Kijiji

***Kiashiria B 4.2 Makadilio ya pesa yaliyopo kwa ajili ya kusimamia msitu wa hifadhi wa Kijiji***

Kwa mahojiano yaliyofanyika kwa wajumbe wa kamati ya maliasili na Serikali ya Kijiji, makadilio ya pesa zilizopo na matumizi kwa kila kamati ya maliasili kwa kijiji ni kama inavyoonyeshwa hapo chini. Kwa ujumla kiasi cha shilingi 7,885,000 ilikua ni pesa kwa vijiji tisa kati ya vijiji kumi vilivyopo. Kijiji cha Likwaya hakijatenga makadilio ya pesa yeyote kwa ajili ya usimamizi wa msitu wa Kijiji

**Jedwali namba 19.** Makadilio ya pesa yaliyopo kwa vijiji kumi kwa ajili ya kusimamia msitu wa hifadhi wa Kijiji

| Kijiji | Makadilio ya pesa kwa kamati ya maliasili ya Kijiji mwezi wa 07/2012 - 6/2013 |
|---|---|
| Kinyope | 1,000,000 |
| Kiwawa | 1,695,000 |
| Likwaya | 0 |
| Makumba | 1,068,800 |
| Milola Magharibi | 200,000 |
| Mkanga1 | 17,000 |
| Mkombamosi | 1,233,000 |
| Muungano | 1,471,200 |
| Nandambi | 500,000 |
| Ruhoma | 700,000 |
| **Total** | **7,885,000** |

**Jedwali namba 20.** Makadilio ya pesa iliyopo ikilinganishwa na kiasi cha pesa kilichotumika kwa kijiji kwa ajili ya kusimamia msitu wa hifadhi wa Kijiji kuanzia mwezi wa 7/ 2012 – 6/ 2013.

| Kijiji | Maelezo ya matumizi yaliyofanyika | | | Kiasi cha pesa kilichobaki |
|---|---|---|---|---|
| Kinyope 1,000,000 | **Vifaa/Shughuli iliyofanyika** | **Idadi** | **Gharama iliyotumika** | |
| | Uandaaji wa katiba ya kamati ya maliasili | 1 | 4,000 | |
| | Usafiri kwa ajili ya kufuatilia katiba mpya Lindi mjini | | 17,000 | |
| | Uandaaji wa katiba mpya | | 47,000 | |
| | Tozo/gharama kwa ajili ya kupeleka katiba Lindi mjini ili isainiwe | | 21,000 | |
| | Gumboots | Jozi 13 | 246,000 | |
| | Ununuzi wa kofia za mvua | Kofia 12 | 24,000 | |

| Kijiji | Maelezo ya matumizi yaliyofanyika | | | Kiasi cha pesa kilichobaki |
|---|---|---|---|---|
| | Posho kwa ajili ya kamati ya ujenzi wa Zahanati na matundu ya vyoo vya shule | | 130,000 | |
| | Nauli na chakula kwa wajumbe wa kamati kwa ajili ya kufuata vifaa vya ujenzi mjini | | 10,000 | |
| | Nauli na chakula kwa wajumbe kwa ajili ya kupeleka pesa kwenye kitabu cha akiba cha kamati ya maliasili | 4 | 40,000 | |
| | Posho kwa ajili ya kufanya doria | | 90,000 | |
| | Mchango kwa ajili ya ujenzi wa choo cha ofisi ya Kijiji | | 95,500 | |
| | Gharama kwa ajili ya kupiga picha za vitambulisho | 4 | 12,000 | |
| | Matengenezo ya baiskeli | 2 | 64,800 | |
| | **Jumla** | | **801,300** | **198,700** |
| Muungano 1,471,200 | Ununuzi wa sanduku la huduma ya kwanza | 1 | 200,000 | |
| | Viatu (Gumboots) | Jozi12 | 192,000 | |
| | Mchango wa ujenzi wa ofisi ya Kijiji | | 100,000 | |
| | Posho kwa wajumbe kwa ajili ya kwenda kufungua kitabu cha akiba | | 102,000 | |
| | Kuchapisha katiba ya kamati | | 6,000 | |
| | Posho kwa ajili ya kupima Hewa ukaa kwenye msitu wa hifadhi wa Kijiji | | 500,000 | |
| | Posho ya wajumbe kwa ajili ya kufuatilia vifaa vya upimaji wa hewa ukaa kwenye akaunti ya akiba mjini Lindi | 3 | 100,000 | |
| | Thamani za ofisini | Kabati1, Meza, Viti 2 | 280,000 | |
| | Ununuzi wa mbao kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Kijiji | 10 | 70,000 | |
| | **Jumla** | | **1,550,000** | **-78,800** |
| Makumba 1,068,800 | Ununuzi wa simu | 1 | 40,000 | |
| | Ream of papers | 1 | 11,000 | |
| | Ununuzi wa vitabu vya stakabadhi | | 25,000 | |
| | Gundi | | 2,000 | |
| | Posho kwa ajili ya kufuatilia vifaa | | 17,000 | |
| | Posho kwa ajili ya doria | | 180,000 | |
| | **Jumla** | | **275,000** | **793,800** |
| Milola Magharibi 200,000 | Pesa iliyoazimwa kwa ajili ya ujenzi wa choo cha ofisi ya Kijiji | | 200,000 | |
| | **Jumla** | | **200,000** | **0** |
| Mkanga1 17,000 | Matengenezo ya baiskeli za kamati ya maliasili ya Kijiji | | 17,000 | |
| | **Jumla** | | **17,000** | **0** |
| Nandambi 500,000 | Posho kwa ajili ya doria | | 200,000 | |
| | Gharama za kufungua kitabu cha akiba | | 250,000 | |
| | **Jumla** | | **450,000** | **50,000** |
| Kiwawa 1,695,000 | viatu (Gumboots) | Jozi 14 | 210,000 | |
| | Filimbi | 12 | 24,000 | |
| | Panga pamoja na nauli | 1 | 36,000 | |
| | Nauli ya katibu kwenda na Kurudi Dar-es-salaam kwa ajili ya ununuzi wa vifaa | 1 | 50,000 | |

| Kijiji | Maelezo ya matumizi yaliyofanyika | | | Kiasi cha pesa kilichobaki |
|---|---|---|---|---|
| | Posho kwa ajili ya doria | | 340,000 | |
| | **Jumla** | | **660,000** | **1,035,000** |
| Mkombamosi (1,233,000) | Posho kwa ajili ya doria | | 540,000 | |
| | Gharama ya kufungua kitabu cha akiba | | 320,050 | |
| | Nauli kwa ajili ya wajumbe wa kamati | | 24,000 | |
| | **Jumla** | | **884,050** | **348,950** |
| Ruhoma 700,000 | Posho kwa ajili ya doria | | 269,000 | |
| | Posho kwa ajili ya mikutano ya kamati | | 211,000 | |
| | Shajala | | 170,000 | |
| | Nauli ya wajumbe wa tatu (3) wa kamati kwenda ofisi ya maliasili wilaya mjini Lindi kwa ajili ya kufuatilia suala la wavamizi wa misitu ya hifadhi kwa ajili ya kilimo wanaotoka kijiji cha Milola Magharibi | | 50,000 | |
| | **Jumla** | | **700,000** | **0** |

***Kiashiria B 4.3 Idadi ya vijiji vyenye mipango ya usimamizi wa misitu na inatekelezwa***
Vijiji 8 kati ya 10 vilikua na mipango ya usimamizi wa misitu katika ngazi ya kijiji wakati wa zoezi la ufuatiliaji mwezi wa 9, 2013. Mipango ya usimamizi wa misitu haikuwepo katika kijiji cha Makumba na Kiwawa. Katika vijiji vyote 10, kamati za maliasili zina mipango kazi na inatekelezwa ikiwemo shughuli za kufanya doria msituni.

## 6) Taarifa ya ufuatiliaji wa masuala hatarishi

### Hatari ya 1. Wawekezaji binafsi kununua maeneo ya misitu katika eneo la mradi na kufyeka kwa ajili ya kilimo

***Kiashiria 1.1 Idadi ya matukio ya kuuza ardhi kwa wawekezaji binafsi wa kutoka nje ya kijiji***
Hakuna mauzo yeyote ya ardhi ya kijiji kwa mwekezaji wa kutoka nje ya kijiji katika kipindi ambacho taarifa hii ilikua inaandaliwa

***Kiashiria 1.2 Eneo la msitu katika eneo la mradi lililouzwa kwa mwekezaji binafsi wa nje kwa matumizi mengine ya ardhi yasiyo ya kuhifadhi misitu***
Hakuna hekta yoyote ya ardhi ya Kijiji kwa vijiji vyote 10 iliyouzwa kwa mwekezaji wa nje kwa ajili ya shughuli nyingine tofauti na yakuhifadhi misitu kama vile ufugaji na uchimbaji madini

### Hatari ya 2. . Migogoro ya ndani baina ya wanakijiji kuhusu haki ya kuingia msituni

***Kiashiria 2.1 Idadi ya matukio ya migogoro inayohusiana na haki ya kuingia msituni kwa kila kijiji kwa mwaka***
Hakuna matukio yeyote ya migogoro baina ya wanaKijiji yaliyotajwa katika vijiji vyote 10 vya mradi kuhusu haki ya kuingia msituni wakati wa utekelezaji wa mradi. Wanajamii wote wana haki sawa katika kutumia rasilimali za misitu zilizopo katika misitu ya ardhi ya Kijiji.

### Hatari ya 3. Rusha katika malipo ya fedha za MKUHUMI kudhoofisha umadhubuti na usawa wa utekelezaji wa MKUHUMI

***Kiashiria 3.1 Idadi ya matukio ya rushwa yanayohusiana na malipo ya fedha za MKUHUMI kwa mwaka; thamani ya fedha zilizohusika na hatua zilizochukuliwa***
Kulitokea mara 1 tukio la rushwa katika Kijiji cha Likwaya. Katika tukio hilo Mwenyekiti wa Kijiji alitoroka na kiasi cha laki tano (500,000) ambazo zilikusudiwa kusaidia manunuzi ya trekta dogo la kijiji (power tiller). Ufuatiliaji wa suala hilo ulifanyika ikiwa pamoja na kutoa taarifa katika kituo cha polisi mkoani Lindi

### Hatari ya 4. Rushwa inayohusiana na usimamizi wa misitu ya hifadhi inaweza kupelekea ufyekaji wa misitu

***Kiashiria 4.1 Idadi ya matukio ya rushwa yanayohusiana na usimamizi wa misitu ya hifadhi***

Kuna tukio moja la uvunaji holela wa mbao limetokea kwa Kijiji cha Kinyope na Muungano.

**Hatari ya 5. Kutokuwepo kwa utashi wa kisiasa katika utekelezaji wa MKUHUMI Tanzania, inaweza kupelelekea utungwaji wa Sheria ambayo itazuia jamii kupata malipo ya moja kwa moja ya fedha za MKUHUMI**

***Kiashiria 5.1 Matamko ya kisera yanaunga mkono au yanazuia wanavijiji kupata fedha za malipo ya MKUHUMI***
Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa MKUHUMI umejumuisha haki ya Jamii ya kupata mapato ya MKUHUMI kama ndio njia sahihi.

**Hatari ya 6. Fedha za MKUHUMI ni kidogo na hazitoshi kutoa motisha ya usimamizi endelevu wa misitu.**

***Kiashiria 6.1 Idadi ya vijiji vilivyokataa kuendelea na mradi kutokana na kutokuridhika na manufaa au mapato yanayotokana na MKUHUMI.***
Hakuna kijiji hata kimoja kilichokataa kuendelea na mradi baada ya malipo yatokanayo na utekelezaji wa MKUHUMI

## 7) Hitimisho

Kwa ujumla mradi umekuwa na athari chanya kwa jamii na bionuwai zilizopo katika maeneo hayo ukulinganisha na bila kuwepo kwa mradi.

Mikakati ambayo imeleta matokeo makubwa kwa watu walio wengi ni pamoja na malipo ya utekelezaji wa MKUHUMI na uwekezaji katika miradi ya maendeleo.

Kujenga uwezo katika kuboresha hali za maisha ya wanajamii na yenyewe pia imeleta athari chanya kwa jamii hasa katika kuiga na kutekeleza mbinu za kilimo bora.